# Afya yako na Ajira

TAARIFA MUHIMU KWA WAFANYIKAZI

## Je, Mfanyikazi anapaswa kufanya nini iwapo ana joto jingi mwilini au dalili zingine?

Iwapo mfanyikazi ataonyesha dalili kama vile kukohoa, joto jingi mwilini, au matatizo ya kupumua anapaswa kujitenga mbali na wengine na papo hapo kuwasiliana na simu ya dharura ya COVID-19 ya Qatar ambayo ni **16000**.

Iwapo kuna dharura, mfanyikazi anapaswa kuitisha gari la wagonjwa kwa kupiga simu ya **999**.

## Mfanyikazi anapaswa kufanya nini iwapo hana kadi ya afya?

Wakati huu wa msukosuko, umiliki wa kadi ya afya na/au QID haihitajiki ili kuweza kupimwa na/au kupokea matibabu. Huduma hizi zinapeanwa bure na Serikali.

## Ni wakati gani mfanyikazi anapaswa kuanza kujitenga-mwenyewe?

Mfanyikazi anapaswa kujitenga-mwenyewe na kupiga simu ya dharura ya COVID-19 ya **16000** iwapo:

- Anaonyesha dalili zozote za COVID-19, kama vile kukohoa, joto jingi mwilini, au matatizo ya kupumua.
- Amesogeleana na yeyote ambaye amepimwa na kupatikana na COVID-19, hata ikiwa wakati wa kusogeleana hakuonyesha dalili za ugonjwa huu.
- Amerejea hivi majuzi kutoka kwa nchi yoyote ambayo imekuwa kuenea kwa ugonjwa huu kwa wingi.

Tafadhali kwa taarifa zaidi, tafadhali rejelea kwa tovuti ya Wizara ya Afya ya Umma www.moph.gov.qa/

## Je, ni wakati gani wafanyikazi watawekwa katika karantini?

Mfanyikazi anaweza kuwekwa kwa karantini na mamlaka za serikali, huku wakingojea matokeo ya vipimo vyao, iwapo inaaminika kwamba huenda wakawa na ugonjwa wa COVID-19 (iwapo wanonyesha dalili zozote au wamesogeleana na yeyote aliyeambukizwa ugonjwa wa COVID-19).

## Je, nini kitatendeka iwapo kipimo kitaonyesha kuwa mfanyikazi ana ugonjwa wa COVID-19?

Mfanyikazi atakayepimwa na kupatikana kuwa na ugonjwa wa COVID-19 atawekwa kwa karantini katika vituo vilivyoko katika eneo la Mukainis na kupewa uuguzi wote wa kimatibabu unaofaa, chakula na malazi bila malipo.

## Je, ni nani anawajibikia maandalizi ya kujitenga kwa hiari au karantini ya wafanyikazi kwenye makazi ya kutumika na watu wengi?

Timu maalum inayofanya kazi chini ya usimamizi wa Kamati Kuu ya Uthibiti wa Msukosuko Huu Chini ya Wizara ya Afya ya Umma inawajibika kwa upangaji wa matibabu ya wafanyikazi waliojitenga kwa hiari na wa karantini. Mwajiri hawajibikii kupanga kujitenga kwa hiari au kwa karantini ya wafanyikazi.

## Je, wafanyikazi wasio na QID inayokubalika watapokea matibabu iwapo yanahitajika?

Wafanyikazi wote watapokea matibabu yote yanayohitajika bila malipo, na hali ya QID yao haijalishi.

## Je, wafanyikazi wangali watalipwa huku wakiwa wamejitenga kwa hiari, kwa karantini au wakipokea matibabu?

Wafanyikazi wote waliojitenga kwa hiari, kwa karantini au wanaopokea matibabu wangali watalipwa mshahara wa kawaida na marupurupu yao bila kujali iwapo wanastahiki kupokea mafao ya likizo ya ugonjwa.

## Je, wafanyikazi walioajiriwa katika sekta ambazo zimefuata maagizo ya serikali ya kusimamisha huduma wangali watapokea mshahara wao wa kawaida na marupurupu mengine kama vile chakula na makao?

Ndio, wafanyikazi wote wanapaswa kupokea mshahara wao wa kawaida na marupurupu kutoka kwa mwajiri wao.

## Je, kandarasi za wafanyikazi zinaweza kusitishwa kutokana na msukosuko wa ugonjwa huu?

Waajiri wana haki ya kusitisha kandarasi.Walakini, usitishaji wa uajiri unapaswa kutekelezwa kwa kuzingatia kikamilifu masharti ya Sheria za Leba na Kandarasi yenyewe, ikijumuisha kipindi cha ilani na malipo yote yanayostahiki ambayo hayajalipwa ikijumuisha tiketi ya ndege ya kurejea nchi ya nyumbani.

## Je, wafanyikazi wanaweza kuombwa watumie likizo yao ya mwaka au wachukue likizo ya bila kulipwa ili kusimamia kipindi ambacho hawataweza kufanyakazi au kutokana na kampuni kupungukiwa na shughuli za kazi?

Ni muhimu kwa wote kushirikiana wakati huu ili kupunguza hasara kwa wahusika wote, kwa kuzingatia hatma ya baadaye ya kazi yenyewe na ajira kwa kipindi cha muda mrefu.

Kwa hivyo, waajiri na wafanyikazi wanaweza kuelewana kwa faida yao pamoja kwamba wafanyikazi wachukue likizo ya bila malipo au kutumia likizo yao ya mwaka, iwapo biashara imesimamishwa na mfanyikazi hajapangiwa kazi yoyote. Walakini, waajiri ni lazima waendelee kupeana yale mafao mengine yote, ikijumuisha na chakula.

## Iwapo wafanyikazi wako nje ya nchi na hawawezi kurudi, Je, hili litaathiri hali yao ya ajira jinsi gani?

Mwajiri na mfanyikazi wanapaswa kujadiliana masharti ya kazi na mafao.Mfanyikazi ana haki ya kikataa marekebisho yoyote kwenye ile kandarasi.Katika hali ya kufutwa kazi, hili linapaswa kutekelezwa kwa kuzingatia kikamilifu masharti ya Sheria za Leba na Kandarasi yenyewe, ikijumuisha kipindi cha ilani na malipo yote yanayostahiki ambayo hayajalipwa.

## Je, Visa na QID zitaongezewa muda kiotomati iwapo muda wa kuisha kutumika utaisha wakati huu wa huduma chache za serikali?

Ili kuongezea muda wa visas (au kuangalia hali yake) fuata kiungo hiki: https://portal.moi.gov.qa/visitvisaextension

Ili kuongezea muda wa QID (au kuangalia hali yake) tafadhali tumia app ya **Metrash2**

Tafadhali rejelea tovuti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ili kupata taarifa za hivi punde zaidi.

## Je, masharti haya yanatumika kwa wafanyikazi wa nyumbani walioajiriwa nyumbani?

Taarifa yote iliyo hapa juu inatumika pia kwa wafanyikazi wa nyumbani walioajiriwa nyumbani.

## Iwapo wafanyikazi wana malalamishi au tatizo kuhusu ajira yao au malazi wakati huu Je, wanaweza kufanya nini?

Wafanyikazi wanapaswa kuwasiliana na Wizara ya Usimamizi wa Maendeleo, Leba na Masuala ya Kijamii kwa nambari ya simu **16008** au kwa barua pepe katika info@adlsa.gov.qa